- (c) katika pahala pengine popote maana yake ni ahadi zilizotolewa mbele ya ofisa wa mambo ya nje ambaye ana uwezo wa kisheria kusimamia kiapo, au mbele ya mtu yoyote ambaye ana uwezo wa kisheria au yule ambaye kwa wakati huo ameteuliwa na Waziri anayehughulikia mambo ya sheria kwa amri katika Gazeti;

"njin" au "barabara" ni pamoja na njia kuu, njia, daraja, sehemu nyengine za kupita pamoja na njia ya miguu ambazo watu wanao uwezo au wameruhusiwa kupita ikiwa kwa malipo au vyenginevyo;

"sheria ndogo" maana yake ni sheria iliyotungwa kwa mujibu wa uwezo wowote aliopewa kisheria mtu yeyote kwa njia ya sheria, taarifa, amri, tangazo, sheria ya mahakama, kanuni, au chombo chengine kilichotungwa chini ya sheria yoyote au uongozi mwengine wa halali;

"maji yaliyomo ndani ya mipaka ya nchi"

(a) inapotumika kuhusiana na Zanzibar maana yake ni sehemu yoyote ya bahari kuu na ambayo inatambuliwa na Serikali na iliyo ndani ya maili fulani kutoka mwambao wa Zanzibar iliyopimwa wakati wa maji kupwa ambayo inatambulika kimataifa chini ya sheria za bahari, na inajumuisha maji yoyote mengine yaliyomo ndani ya Zanzibar;

(b) inapotumika kuhusiana na Jamhuri ya Muungano maana yake ni maji yoyote ya nchi na ambayo yanatambuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kama inavyotambuliwa kimataifa chini ya sheria za bahari na inajumuisha maji yaliyomo ndani ya Jamhuri;

"Hazina" maana yake ni Waziri anaehusika na mambo ya fedha na ofisa mwengine au wengine wa Wizara yake ambao watawekwa na yeye kufanya kazi kwa niaba ya Hazina kufuatana na uwezo au kazi yoyote iliyocainishwa au kulazimishwa Hazina kuitenda kwa mujibu wa sheria yoyote;

"mwasiliano ya mbali" maana yake ni matangazo yoyote, ujumbe, su upokeaji wa ishara, alama, maandishi, sura su sauti au upelelezi wa umbile lolote kwa waya, redio, vyombo vya kuones au vyombo vyengine vya electromagnetiki, uneme au smaku;

"Siku ya Muungano" maana yake ni siku ya 26 ya mwezi wa Aprili, 1964;

"Dola ya Uingereza" maana yake ni Uingereza na Ireland ya Kaskazini;

"Jamhuri ya Muungano" maana yake ni Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar;

"chombo" ni pamoja na meli yoyote au mashua au chombo chochote chengine kinachotumika katika safari za majini;

"Makamo wa Rais" maana yake ni Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano;

"usia" inajumuisha na usia wa nyongeza;

"maandishi" au neno lolote lenye maana hiyo ni pamoja na maneno yaliyochapishwa, yaliyopigwa chapa, kuchorwa, yaliyopigwa picha au yaliyowakilishwa au kutolewa tena katika sura ya kuonekana;

"sheria iliyoandikwa" maana yake:-

- (a) sheria zote pamoja na sheria za Jumuiya ambazo zinatumika katika Zanzibar kwa wakati huu;
- (b) sheria yoyote ndogo ambayo inatumika katika Zanzibar kwa wakati huu; au
- (c) sheria iliyokubalika pamoja na masahihisho yoyote yanayohusika na ambayo inatumika Zanzibar kwa wakati huu;

"mwaka"

- (a) unapotumika kuhusiana na mwaka wa kalenda maana yake ni kipindi kinachoanzia siku ya mwanzo ya mwezi Januari hadi siku ya thelathini na moja ya mwezi Disemba ya mwaka huo;
- (b) unapotumika kuhusiana na mwaka mmoja maana yake ni kipindi chochote cha miezi kumi na mbili mfululizo;

"Zanzibar" maana yake ni Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na vijisiwa vidogo vidogo vilivyo katika Bahari ya Zanzibar, na pale "Zanzibar" inapotumika kijiografia maana yake ni yale mseneo ambayo kwa pamoja hapo zamani yalikuwa yakijuilikana kwa jina la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

SEHEMU YA III

Sheria kila siku inajieleza.

5. Sheria ni lazima ifahamike kwamba kila siku inajieleza, na wakati wowote umbo au vitu vinapoelezwa katika wakati wa sasa, ni lazima itumike katika mazingira yatakayotokea, ili kwamba umuhimu uwekwe katika hiyo sheria na katika kila sehemu yake kulingana na makusudio, nia na maana yake.

Sheria inajaaliwa kujirekebisha.

6. Kila sheria ionekane kwa njia inayoweza kujirekebisha na ipewe tafsiri hiyo, pamoja na uchambuzi ambao kwa kiwango kikubwa kabisa utahakikisha kupatikana kwa malengo yaliyokusudiwa na chombo cha kutunga sheria.

Sheria zilizopo
zitumike baada
ya mareke-
bisho n.k.
hadi ziondo-
shwe ama
kusawazishwa.

7. Sheria zilizokuwa zikitumika mpaka kabla ya tarehe kumi na moja Januari, 1964 zitaendelea kutumika na zitakuwa na marekebisho fuleni, maingizo au mapunguzo ambayo yatahakikisha kupatikana kwa mazingara ya kisasa kama itarajiwavyo.

Majina ya
samani
yatafsiriwe
kwa
kulingana
na wakati.

8. (1) Bila ya kuathiri sheria yeyote iliotungwa na chombo cha kutunga sheria:-

- (a) ikiwa sheria ya zamani yeyote inataja Sultani au Waziri Mkuu aliyepita basi isomeke na ieleweke kuwa ni maana ya Raisi;
- (b) ikiwa sheria ya zamani yoyote inataja "British Resident" au "Resident in Council" basi isomeke kuwa na maana ya Waziri ambae ni mdhamana wa suala hilo katika wakati huu;
- (c) isipokuwa ikiwa, pale sheria hizo za Sultan aliyekuwepo, Waziri Mkuu "British Resident" au "Resident in Council" au "Chief Secretary" zinahusu watu wengine zaidi ya wale waliotajwa hapo juu kwenye 1(a), (b) na (c) isomeke na ieleweke kwa wadhifa huo mwengine ambae, kwa tafsiri ilivyo, ndivyo inavyoeleweka.

(2) Maelezo yoyote katika sheria yoyote yahusuyo "Protectorate" yasomeke kuwa yanahusu Zanzibar.

Utangulizi.

9. Utangulizi wa sheria haitakuwa ni sehemu ya sheria lakini itawajibika kusomwa kama ni kitu kilichokusudiwa kusaidia kufafanua madhumuni na malengo yake ya sheria hiyo.

Jina kamili
na jina dogo.

10. Jina kamili na jina dogo la sheria hayatakuwa ni sehemu ya sheria, lakini yasomeke kama ni sehemu ambazo zimekusudiwa kusaidia katika kufafanua madhumuni na kwa ajili ya kukariri tu.

Maandishi
pembeni mwa
mstari na
maelezo
kuhusu sheria
iliyopita.

11. Maandishi yaliyo pembeni mwa mstari na maelezo kuhusu sheria iliyopita hayatakuwa sehemu ya sheria, lakini yatahesabika kuwa yameingizwa kwa faida ya kukariri tu.

Uka/uume
na nambari.

12. Katika sheria yoyote, isipokuwa kinyume cha maana kionekane:-

- (a) maneno yatumiayo mwanamme pia yanahusu mwanamke;
- (b) maneno yatumiayo mwanamke pia yanahusu mwanamme;
- (c) maneno katika umoja pia yanajumuisha uwingi na maneno katika uwingi pia yanajumuisha na umoja.

Matumizi
ya vifungu
vya
ufafanuzi.

13. (1) Maana au kanuni za ufafanuzi zilizomo katika sheria zinatumika katika ufafanuzi wa vifungu vya sheria vinavyohusika pamoja na sheria nzima.

(2) Pale ambapo sheria inacho kifungu cha ufafanuzi, isomeke na kueleweka:-

- (a) kuwa utatumika tu pale ambapo hapatokuwako na mgongano na sheria wenyewe;
- (b) kuwa utatumika kwa sheria zote nyengine zinazohusiana na mada hiyo isipokuwa kama lengo jengine litaonekana.

Maneno
katika
kanuni.

14. Pale sheria inapotosa uwezo wa kuunda kanuni, maelezo yatakayotumika katika kanuni hizo yanakuwa na maana ile ile kama ilivyo katika sheria iliyotosa uwezo huo.

Maelezo
kuhusu
masafa.

15. Katika upimaji wa masafa yoyote kuhusiana na sheria, ila pale sheria inapohitajia vyenginevyo, masafa hayo yatapimwa kwa mpango wa usawa (straight line) katika usawa uliolala (horizontal plane).

Sehemu za
msembo.

16. Pale iwapo neno limetafsiriwa basi sehemu nyengine ya neno hilo litatafsiriwa kwa mujibu wa msembo ulivyo.

SEHEMU YA IV

MATUMIZI YA SHERIA ZA MUUNGANO KWA ZANZIBAR

Sheria za
Muungano.

17. (1) Hakuna sheria yoyote itakayopitishwa na Bunge la Muungano ambayo itatumika Zanzibar mpaka sheria hiyo iwe ni kwa ajili ya mambo ya Muungano tu na ipitishwe kulingana na maelekezo yaliyo chini ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Sheria kama hiyo lazima ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika.

Sheria ndogo.

18. Pale sheria ndogo inapoundwa kwa mujibu wa uwezo uliotolewa na sheria hii chini ya kifungu cha 17 (1) na (2) sheria hii itatumika tu pale itakapotimiza shuruti zote zilizowekwa kwa matumizi ya sheria mama (parent act) kama ilivyoainishwa katika kifungu hiki.

SEHEMU YA V

VIFUNGU VINAHUSIANA NA SHERIA

Sheria ziwe
za umme
kutambulika
mahakamani.

19. Kila sheria ni sheria ya umma
na inatambulika mahakamani kama ilivyo isipokuwa
kama kuna kitu kinachoonesha kinyume chake.

Kifungu kuwa
sheria
kamili.

20. Kila kifungu cha sheria kitakuwa
na maana pekee bila ya maneno ya nyongeza
au vianzio.

Uandishi na
unukuuji wa
sheria.

21. Wakati sheria inapotajwa, itakuwa
inatoshesheleza kwa shughuli zote:-

- (a) kuiita sheria hiyo kwa jina dogo,
kama lipo, ambalo limeelezwa
kuwa ndilo hilo au;
- (b) kuiita sheria hiyo kwa jina lake
kamili, au
- (c) kuiita sheria hiyo kwa mwaka ambao
ilitoka na nambari ya sheria hiyo
katika jumla ya sheria zilizotoka
mwaka huo; au
- (d) katika toleo jipya (revised edition)
lililosahihishwa sheria hiyo kwa
jina fupi au kwa nambari ya sura
ya sheria hiyo isipokuwa tu inaweza
kuwa maelezo yawe ni kwa mujibu wa
nakala za sheria zilizochapishwa
na wachapishaji wa Serikali.

(2) Jina la au maelezo kuhusu sheria
fulani litahesabiwa kuwa ni jina la au maelezo
ya sheria ambayo imesahihishwa.

Mipaka ya
matumizi.

22. (1) Kila sheria inatumika kwa Zanzibar yote isipokuwa ikiwa itaelezwa vyenginevyo ndani ya sheria hiyo.

(2) Pale ambapo sheria isiyotumika katika Zanzibar nzima itarekebisha, hakuna kifungu katika sheria hiyo mpya kitachotumika katika sehemu yoyote ya Zanzibar ambayo haikuhusika na sheria ile ya mwanzo (iliyorekebisha), isipokuwa kama itaeleza yenyewe kwamba marekebisha hayo yataihusu sehemu ya Zanzibar au Zanzibar nzima.

Tarehe ya
kuanza
kutumika.

23. (1) Katibu wa Baraza la Wawakilishi ataingiza katika kila sheria, mara tu baada ya jina la sheria hiyo, siku, mwezi na mwaka ambapo sheria hiyo imepitishwa chini ya jina la Rais na maandishi hayo yatachukuliwa kuwa ni sehemu ya sheria, na tarehe ya idhini hiyo itakuwa ndiyo tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hiyo ikiwa hakuna tarehe nyengine iliyowekwa kuanza kutumika.

(2) Ikiwa sheria yoyote au sehemu ya sheria imeelezwa kuwa imeanza, au itaanza kutumika katika tarehe fulani maalum, itahesabiwa kuanza mara tu pale siku iliyoitangulia siku iliyotajwa itakapomalizika.

(3) Ikiwa imeelezwa katika sheria yoyote kwamba itaanza kutumika katika tarehe fulani ambayo Rais au Waziri ataituwa kwa tangazo katika Gazeti, na ikiwa Rais au Waziri kwa tangazo katika Gazeti ataituwa tarehe hiyo itakuwa halali kwa Rais au kwa Waziri katika wakati wowote kabla ya tarehe iliyotangazwa kuifuta tarehe hiyo kwa tangazo jengine na kuteuwa tarehe nyengine.

Sheria kuacha kutumika.

24. Iwapo sheria imeelezwa siku ya kumalizika muda au kutoweza tena kufanya kazi katika siku maalum, itahesabiwa kuacha kutumika kuanzia siku inayofuatia baada ya siku hiyo kufika.

Uwezo unaoolewa wa kurekebisha.

25. Pale sheria inapotoa uwezo wa kutunga:-

- (a) kanuni au sheria ndogo ndogo;
- (b) amri au sheria ndogo kutengenezwa na vyombo vya sheria, ina maana isipokuwa kinyume chake kionekane, ni uwezo unaoviwzesha katika utaratibu huo huo na kufuatana na shuruti au mipaka hiyo hiyo, kufuta, kurekebisha au kuunda tena kanuni hizo zilizoundwa chini ya uwezo huo.

Kufuta sheria iliofuta.

26. Pale sheria itapofuta sheria nyengine iliyofuta sheria, sheria hiyo mpya haitengenezi sheria nyengine ambayo imeondolewa isipokuwa kama yataingizwa maneno kuonesha hivyo.

Athari ya kufuta na mambo ya ujumla.

27. (1) Bila ya kuingilia kifungu cha 26, pale sheria inapofuta sheria nyengine, nusu ama yote, sheria hiyo mpya isipokuwa kinyume chake kionekane, haikusudii:-

- (a) kufufua kitu chochote ambacho hakina nguvu katika wakati ambapo sheria mpya inanza kutumika;
- (b) kuathiri kazi zilizopita za sheria iliyoondoshwa au kitu chochote kilichoathirika na sheria hiyo;
- (c) kuthiri haki zozote, fursa, majukumu au makosa yanayopatikana, yanayotokea au yaliyotokea chini ya sheria iliyoondoshwa; au

- (d) kusthiri adhabu yoyote, ya utaifishaji au adabu iliyotolewa kutokana na kosa lolote lililofanywa kinyume na kifungu kilichofutwa; au
- (e) kusthiri upelelezi wowote, mashtaka au daawa au haki kutokana na haki hiyo, fursa, majukumu, kosa, adabu, kutaifisha au adhabu; na upelelezi wa sina hiyo au mashtaka inaweza kuanzishwa, kuendelezwa au kutiliwa nguvu, na adhabu yoyote ya utaifishaji au adhabu inaweza kutekelezwa kama kwamba sheria mpya haijapitishwa.

(2) Kifungu hiki kinahusu kumalizika muda kwa sheria ya muda kama kwamba imefutwa na sheria nyengine.

Athari ya kufutwa kwa sheria kwenye sheria ndogo.

28. Pale ambapo sheria yoyote au sehemu ya sheria imefutwa na kuundwa tena kwa sheria nyengine, sheria ndogo iliyoundwa chini ya sheria au sehemu ya sheria ambayo imefutwa isipokuwa kinyume chake kionekane, itaendelea kutumika iwapo tu haipingani na vifungu vya sheria mpya, mpaka pale ambapo sheria ndogo hiyo itakapopingwa na sheria ndogo nyengine, iliyoundwa chini ya sheria mpya au sehemu ya sheria mpya, na mpaka pale ambapo kufutwa huko kutakuwa ni kwa halali kwa mujibu wa vifungu vya sheria mpya.

Sheria inaweza kubadilishwa, au kufutwa katika kikao hicho hicho.

29. Sheria inaweza kubadilishwa, kusahihishwa, au kufutwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi ambacho kiliipitisha.

Tafsiri ya sheria inayosawazisha na inayosawazishwa.

30. Pale sheria moja inayosawazisha sheria nyengine sheria inayosawazisha, maadam tu haitafautiani na isipokuwa nia tofauti ionekane, itafsirike kama ni moja na sheria inayosawazishwa.

Uchapishaji
wa sheria
mpya.

31. Ikiwa sheria imesahihishwa, itakuwa ni halali kwa wachapishaji wa Serikali, kwa idhini ya Mwanasheria Mkuu, kutoa nakala za sheria pamoja na kuongeza maongezo mengine muhimu, kupunguza, kubadilisha na matengenezo yatakayosababishwa na sheria mpya na nakala kama hizo zitahesabika kuwa ni nakala sahihi za sheria hiyo iliyorekebishwa.

Maelezo
kuhusu
sheria
iliyore-
kebishwa.

32. Pale ambapo katika sheria inanukuu sheria nyengine yoyote ilioandikwa, maelezo hayo, isipokuwa pale maana itakavyohitaji vyengine, yatahesabika kuwa ni maelezo kuhusiana na sheria hiyo iliyoandikwa kama itavyorekebishwa wakati hadi wakati.

Kumukuliwa
kwa mara
mbili
ambako sheria
imeandikwa
upya au
kupitiwa.

33. Pale sheria inapokuwa na maelezo kuhusiana na kifungu chochote cha sheria iliyoandikwa ambayo imefutwa na kuundwa tena, au sheria halisi iliyorudiwa ambayo imechapishwa, maelezo ya namba hiyo yatafsiriwe kuhusiana na kifungu mkabala (corresponding provision) cha sheria ambayo imeundwa tena, au iliyopitiwa.

Maelezo
kuhusu sheria
ni pamoja na
sheria ndogo.

34. Maelezo yoyote kuhusiana na sheria katika sheria yoyote inajumuisha maelezo ya sheria ndogo yoyote iliyoandikwa chini ya sheria ambayo maelezo yametoka.

Sheria iwapo
haitatumika
baada tu ya
kutungwa.

35. Pale ambapo sheria haitatumika mara tu baada ya kutungwa inatowa uwezo wa kuteuwa au kufanya sheria ndogo au kitu chengine chochote kwa madhumuni ya sheria hiyo, uwezo huo unaweza ila iwapo maelezo yahitajia vyenginevyo, itafanywa wakati wowote baada ya sheria hiyo kutungwa kwa kiwango kile ambacho ni lazima au muhimu kwa madhumuni ya kufanya sheria hiyo itumike katika tarehe ya kuanza, kwa kuzingatia kwamba uteuzi wowote au sheria ndogo au kitu chengine chochote kilichofanywa, kutolewa au kutendwa chini ya nguvu hizo, ila iwapo maelezo yanahitajia vyenginevyo, au ila iwapo kitendo hicho, au sheria ndogo hiyo

ni lazima kwa kufanya sheria hiyo itumike hakitokuwa na nguvu yeyote ila hapo sheria itapoanza kutumika.

SEHEMU YA VI

VIFUNGU VINAVYOHUSU SHERIA NDOGO

Uchapishaji
wa sheria
ndogo.

36. Sheria ndogo zote isipokuwa iwe imeelezwa vyenginevyo katika sheria hiyo au imehusiana na uteuzi wa mtu yoyote katika ofisi yoyote au imehusiana na jambo lolote lisilokuwa na nguvu ya kisheria, zitachapishwa katika Gazeti na zitatambuliwa mahakamani.

Tarehe ya
kuanza
kutumika
sheria ndogo.

37. Sheria ndogo yoyote iliyochapishwa katika Gazeti itaanza kutumika katika siku ambayo ilichapishwa au, ikiwa imeainishwa ama katika sheria ndogo hiyo au kifungu chengine chochote itaanza kutumika katika tarehe nyengine, sheria ndogo kama hiyo au, kifungu cha namna hiyo, na bila kuathiri kifungu cha 38, itaanza kutumika katika tarehe hiyo nyengine.

Kutumika
kwa sheria
ndogo kabla
ya tarehe ya
kuchapishwa.

38. Sheria ndogo yeyote inaweza kuundwa na kufanya kazi kuanzia tarehe ya nyuma, ambayo siyo tarehe ya nyuma zaidi ya tarehe iliyoanza kutumika sheria yenyewe ambayo hiyo sheria ndogo imezaliwa nayo.

Kwa kuzingatia kwamba mtu yoyote hawezi, isipokuwa iwe imeelezwa wazi katika sheria hiyo, kufanywa au kuhesabika na makosa yoyote yale kuhusiana na kosa, tendo lolote lilifanywa au kuscha kufanywa kitu chochote kabla ya tarehe ambayo hiyo sheria ndogo imechapishwa Gagetini.

Ufafanuzi wa sheria ndogo.

39. Pale sheria inapotoa uwezo wa kutunga sheria ndogo yoyote, maelezo yaliyotumika katika sheria ndogo itakuwa, isipokuwa pale kinyume cha madhumuni hayo kionekane, na maana sawa kama ilivyo katika sheria iliyotos uwezo huo, na maelezo yoyote katika sheria hiyo ndogo kuhusiana na "sheria" itakuwa na maana ya ile sheria inayotoa uwezo wa kuunda sheria ndogo ya aina hiyo.

Vitendo vilivyofanywa chini ya sheria ndogo vitahesabika kuwa ni vya sheria iliyounda sheria ndogo.

40. Tendo au kitu kilichofanywa chini ya au kufuatana na, au kwa sababu ya, sheria ndogo yoyote yatahesabika kuwa yemtendeka chini au kufuatana na au kwa sababu ya sheria ambayo imetoa uwezo wa kuunda sheria ndogo hiyo.

Jina la sheria ndogo.

41. Sheria ndogo inaweza kuitwa kwa kutumia jina dogo, kama lipo, au kwa kumbukumbu ya namba ambayo lilichukua katika tangazo la Gazeti.

Vifungu kuhusiana na uwezo wa kuunda sheria ndogo.

42. Pale sheria yoyote inapotoa uwezo kwa chombo chochote kuunda sheria ndogo, vifungu vifuatavyo ili iwapo maelezo yahitaji vyenginevyo vitakuwa na nguvu kutokana na kufanya sheria hiyo ndogo:-

- (a) pale sheria ndogo yoyote itakapopewa imeundiwa kufuatana na uwezo fulani itahesabika pia kuwa imeundwa au kutolewa kuhusiana na uwezo wote ambao umewekwa na unao nguvu;
- (b) kifungu chochote cha sheria ndogo ambacho kinapingana na kifungu chochote cha sheria ambayo ndiyo iliyounda hiyo sheria ndogo kitakuwa hakina maana (hakifai) kwa sababu kinapingana;

- (c) sheria ndogo inaweza wakati wowote kurekebishwa, kupingwa au kuondeshwa na chombo kile na katika msingi ule ule ambao imetungwa.

Isipokuwa kwamba iwapo uongozi wa namna hiyo umebadilishwa wote au nusu na uongozi mwingine, uwezo ulioainishwa hapa unaotokana na uongozi wa awali unaweza kuchukuliwa na uongozi mpya katika mambo yote au vitu vyote vilivyo katika uwezo wake kama kwamba ni ule uongozi wa awali;

- (d) pale sheria yoyote inapotosa uwezo kwa chombo chochote kuunda sheria ndogo kwa matumizi yoyote ya kijumla, na pia kwa matumizi yoyote maalum ambayo kwa bahati yashusika nayo, basi maelezo ya madhumuni hayo hayatochukuliwa kukiuka uwezo wa chombo hicho chenye uwezo huo;

- (e) kutakuwa na dhabu kwa kosa lolote la kukiuka sheria ndogo, na adhabu hiyo haitosidi faini ya shilingi elfu saba au kifungu kisichoziidi miaka miwili au vyote faini kama hiyo na kifungo kama hicho. Kufuatana na vile itavyoonekana sawa na kila chombo kilichotunga sheria ndogo hiyo.

Iwapo kwamba hakuna adhabu nyengine iliotolewa chini ya sheria mama.

Ada.

43. (1) Pale sheria yoyote inapotoa uwezo kwa mtu yoyote kuunda sheria ndogo na kuunda vifungu ndani yake vinavyohusiana na ada au malipo mengine, sheria ndogo ya namba hiyo insweza kueleza mambo yote au machache kati ya haya yafuatayo:-

- (a) ada au malipo maalum;
- (b) ada au malipo ya juu kabisa au ya chini kabisa;
- (c) ulipeji wa ada au malipo iwapo ya kijumla ama chini ya shuruti maalum au katika mazingira maalum; na
- (d) upunguzaji, ukiukaji au malipo ya marejesho ya kijumla au sehemu ya ada au malipo yoyote, ama kwa kuzuka kwa tokeo fulani au kusababishwa na mtu fulani.

(2) Pale upungufu wowote, ukiukaji au marejesho kwa jumla au ya sehemu, wa ada au wa malipo yoyote imeainishwa, upungufu wa namba hiyo ukiukaji au marejesho unaweza kuelezwa kwamba utatumiwa au utatumika ama kuwa kijumla au kwa shughuli maalum:-

- (a) kuhusiana na mambo fulani au mikataba au vikundi vya mambo fulani au vikundi vya mikataba fulani;
- (b) kuhusiana na nyaraka fulani au vikundi fulani vya nyaraka;
- (c) wakati tukio lolote linapotokea au kusita kutokea;
- (d) kuhusiana na watu fulani au makundi fulani ya watu; au

- (e) kuhusiana na mchanganyiko wowote wa mambo, mikataba, nyaraka, matukio au watu; na unaweza kuelezwa kwamba unatumika au utatumika kutokana na shuruti za namba hiyo kama zitakavyodhihirishwa katika sheria ndogo au katika maoni ya mtu yoyote aliyeainishwa ndani yake.

SEHEMU YA VII

KUHESABU WAKATI

Wakati.

44. (1) Nyakati sahihi za Zanzibar zitakuwa ni saa tatu zaidi ya wakati wa Uingereza (GMT).

(2) Pale maelezo yoyote kuhusu wakati katika sheria, waranti au kitu chochote, wakati utakaotumiwa isipokuwa iwe imeelezwa vyengine, utakuwa ni wakati sahihi wa Zanzibar.

Hesabu ya wakati.

45. Katika kuchunguza wakati kuhusiana na sheria yoyote, isipokuwa ikiwa itaelezwa vyenginevyo:-

- (a) kipindi cha siku baada ya tukio fulani au baada ya kutendwa tendo lolote au kitu chochote kitahesabika kutoijumlisha ile siku ambayo tukio limetokea au tendo au kitu kimetendeka;
- (b) ikiwa siku ya mwisho ya kipindi ni Jumapili au ni sikukuu (siku ambazo katika kifungu hiki zinaitwa ni siku zisizohesabika) kipindi hicho kitajumuisha siku inayofuata ambayo itahesabiwa;

(c) pale tendo lolote au shtaka ikiwa limekusudiwa au kuruhusiwa kufanywa au kuchukuliwa katika siku fulani, hapo ikiwa siku hiyo imetokea kuwa ni siku isiyohesabika, kosa hilo au shtaka litahesabiwa kutekelezwa kwa wakati upasao ikiwa litatekelezwa katika siku inayofuata ambayo siyo siku isiyohesabika;

(d) pale tendo au shtaka limekusudiwa au kuruhusiwa kufanywa au kuchukuliwa katika kipindi chochote kisichozidi siku sita, siku zisizohesabika hazitohesabiwa katika kuhesabu siku.

Ikiwa wakati haukutaajwa.

46. Pale iwapo hakuna wakati uliowekwa au kuruhusiwa kitu chochote kufanywa, kitu hicho kitekelezwe bila ya kuchelewa, na mara kwa mara kama itavyochitajika.

SEHEMU VIII

VIFUNGU VYA JUMLA KUHUSIANA NA MASHTAKA NA ADHABU

Ushahidi wa sahihi ya Rais, Waziri au Mwanasheria Mkuu kutoa idhini.

47. Pale inapokuwa idhini ya Rais, Waziri au Mwanasheria Mkuu ni muhimu kabla ya kufungua mashtaka au kuanza kitendo chochote, waraka wowote utakeokuwa na idhini ya Rais, Waziri au Mwanasheria Mkuu utepokewa kama ni ushahidi wa moja kwa moja katika mashtaka yoyote bila ya ushahidi kutolewa kwamba sahihi iliyomo katika idhini hiyo ni ya Rais, Waziri au Mwanasheria Mkuu.

Mashtaka ya kiofisa hayafutiki baada ya kifo n.k.

48. Mashtaka yoyote ya hukukia au ya jinai yalichukuliwa kwa au dhidi ya mtu yeyote kuhusiana na ofisi yake hayatafutwa au kusitizwa kutokana na kifo chake, kujiuzulu au kutokuwepo au kuondoshwa kutoka kwenye ofisi, lakini yanaweza kuendelezwa kwa au dhidi ya, kwa vyovyote iwavyo, ya yule mtu ambaye atashika ofisi hiyo kwa wakati huo.

Adhabu
haizuii
mashtaka
ya hukukiya.

49. Kutolewa adhabu au faini kwa au chini ya sheria yoyote hakutofanya, ila iwapo maelezo yanahitaji vyenginevyo mtu yoyote asishtakiwe kujibu mashtaka kuhusiana na hasara aliyosababisha kwa mtu yeyote aliyeumizwa au kuathiriwa.

Vifungu vya
makosa chini
ya sheria
mbili au
zaidi.

50. Pale iwapo tendo lolote au kuacha kutenda chochote kunakuwa ni kosa basi ila maelezo yahitajia vyenginevyo katika sheria mbili au zaidi, mkosaji, itabidi ashtakiwe na kutiwa adabu chini ya sheria yeyote kati ya hizi, lakini hatoshtakiwa na kutiwa adabu mara mbili kwa kosa moja.

Kurekebishwa
kwa adhabu.

51. Pale ambapo kutenda au kuacha kutenda kunahesabika kuwa ni kosa na adhabu ya kosa hilo limerekebishwa baina ya lilipotendeka kosa hilo na pale mtendaji alipoonekana kuwa na hatia, mkosaji, stapewa adhabu ile iliyokuwepo wakati alipotenda kosa hilo ila iwe sheria imeelezea vyenginevyo.

Adhabu
zilizowekwa
zinaweza
kupunguzwa.

52. (1) Ikiwa katika sheria yoyote adhabu imewekwa kwa ajili ya kosa fulani katika sheria hiyo kifungu hicho kitakuwa, isipokuwa kinyume chake kionekane, na maana kwamba kosa hilo litapewa adhabu isyozidi ile iliyowekwa.

(2) Pale ikiwa katika sheria yoyote adhabu zaidi ya moja imewekwa kwa kosa hilo, matumizi ya neno "na" isipokuwa kinyume chake kionekane, yatakuwa na maana kwamba adhabu hizo zinaweza kutolewa moja baada ya moja au zote kwa pamoja.

Kuondosha
kilichota-
ifishwa.

53. (1) Iwapo mnyama yoyote au kitu kimetangazwa na sheria yoyote, au ikiwa yupo au kipo chini ya sheria yoyote ambalo mahakama au chombo chengine kimeamua kitaifishwa, kama hakuna kifungu chengine kinachoeleza vyenginevyo kitachukuliwa na Serikali, na fedha itakayopatikana, ikiwa imeamriwa kiuzwe na chombo chenye uwezo huo, fedha hiyo italipwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ila iwe kuna sheria nyengine inayoелеzea namna ya kufanywa.

(2) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachoathiri kifungu chochote katika sheria yoyote ambapo sehemu yoyote ya faini au kilichotaifishwa kitalipwa kwa mtu yeyote anaehusika.

Utoaji wa
faini na
adhabu.

54. Faini yoyote au adhabu iliyowekwa na au chini ya sheria yoyote, italipwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ila pale itapoelezewa vyenginevyo.

Sheria
kuhusu
jaribio.

55. Katika sheria yoyote kifungu kinachohusiana na jaribio kitachukuliwa kama ni jaribio la kufanya kosa chini ya kifungu hicho, na adabu itatolewa kama kwamba kosa halisi limetendeka.

Pale kosa
linapofanywa
na Shirika.

56. Pale kosa chini ya sheria yoyote ikiwa limetendwa na Shirika, mtu yeyote ambaye, wakati wa kutenda kosa hilo, alikuwa anahusika akiwa ni Mkurugenzi au Ofisa, anayeshughulika na utawala au uendesheji wa shughuli za Shirika hilo atakuwa na makosa na ataahtakiwa na kutiwa adhabu ipasavyo, isipokuwa ikiwa ataithibitishia mahakama kwamba hakuwa akielewa, na wala hawesi kuelewa, kwa kutumia uwezo alionao wa kutambuwa utendaji wa makosa hayo, isipokuwa tu pale maelezo yatavyoelezea vyenginevyo.

Kosa la
muajiri
au mkuu
wa sehemu.

57. Pale kosa lolote chini ya sheria yoyote linapotendwa na mtu ambaye ni mjumbe au mwajiriwa, isipokuwa ionekane vyengine, pamoja na mjumbe au mwajiriwa, huyo mwakilishwa au mwajiri pia atakuwa na makosa na stashtakiwa na kuhukumiwa ipasavyo isipokuwa kama itathibitishwa na kuiridhisha mahakama kwamba hakuwa akielewa, na wala hawezi kwa kutumia uwezo alionao wa fahamu, kutambua utendaji wa makosa hayo.

SEHEMU YA IX

KUFARIKI, KUCHAGULIWA, KUSTAAFU KWA RAIS
NA UWEZO WA MAOFISA

Kufariki
kwa Rais
n.k.

58. Pale kifo cha Rais kinapotokea au anapojiuzulu si lazima kwa sababu ya kutokea kifo hicho au kujiuzulu huko mtu yoyote anayeshikilia wadhifa wowote kuteuliwa tena au kwamba aspishwe tena ingawa kabla ya kifo hicho ameshakula kiapo cha utifu.

Uwezo wa
Rais wa
muda
kuschisha
au kuajiri.

59. Pale kinapotokea kifo cha Rais au anapojiuzulu na mtu mwengine anaposhika dhamana ya kuwa Rais wa muda:-

(a) Rais huyo wa muda hawezi kumuondosha au kumsimamisha kazi mtu yeyote aliyechaguliwa na Rais aliyefariki mpaka utakapofika wakati ambapo yeye, au mtu mwengine atakapochaguliwa kuwa Rais;

(b) Rais huyo wa muda anaweza kumteua mtu yeyote kushika dhamana ya ofisi ya aina yoyote kulingana na uwezo wa Rais aliyefariki au aliejiuzulu aliyopewa na Katiba au sheria yoyote nyengine na uteuzi huo utatambulika kama kwamba unefanywa na Rais na ataendelea kufanya kazi.

hata baada ya uchaguzi wa Rais
mwengine isipokuwa kama Rais
aliyechaguliwa atamwachisha
kazi au ataamriisha vyenginevyo
kwa mujibu wa aya (a) hapo juu.

Maofisa wa
Serikali
kushika
dhamana
kulingana
na
mapendekezo.

60. Ofisa yeyote wa Serikali aliyeteuliwa
chini ya kifungu cha sheria yoyote, au mtu
yeyote mwenye dhamana ya ofisi chini ya vifungu
vya Katiba atakuwa na dhamana ya ofisi hiyo
katika muda staopenda yule aliyemteua, isipokuwa
ikiwa itaelezwa vyenginevyo katika sheria au
katika Tume au uteuzi wake.

Malipo.

61. Pale mtu anapoteuliwa kushika dhamana
ya ofisi, kile chombo kilichomteuwa kinaweza
kuweka, kubadilisha au kuondosha malipo yake,
ila tu iwe malipo hayo yamewekwa kisheria na
hayabadiliki.

Tarehe ya
kuanza au
kusimamishwa
kazi.

62. Pale mtu anapopewa dhamana ya ofisi na
ikaelezwa kuwa dhamana hiyo itaanza kutumika katika
tarehe fulani maalum, au pale ambapo dhamana ya
mtu inaposimamishwa katika tarehe fulani maalum,
uteuzi au usimamishwaji huo vyovyote iwavyo,
utahesabika mara tu inapomalizika ile siku ya
nyuma yake.

Maneno
ysidhini-
shaji
kuteuliwa.

63. (1) Maneno yanayoidhinisha kuteuliwa
kwa mtumishi wa Serikali kushika dhamana katika
kipindi hicho inajumuisha uwezo wa:-

- (a) kumuachisha au kumwondosha au
kumsimamisha;
- (b) kuteuliwa au kumweka tena na;
- (c) kumteua mwengine badala yake au
kufanya kazi badala yake,

ni miongoni mwa uwezo ambao chombo ambacho kimepewa
uwezo wa kuteua upo.

(2) Maneno yanayomtaka au kumpa uwezo Waziri kufanya kitendo au kitu, au vyenginevyo yanayomhusu kwa mujibu wa wadhifa wake, ikiwa ni pamoja na Waziri (anayemwakilisha) anayefanya kazi chini yake, au ikiwa ofisi iwazi, Waziri aliyekusudiwa kuchukua dhamana ya su chini ya amri ya Rais, na pia pamoja na wataofuata lakini haijumuishi msaidizi wake.

(3) Maneno yanayomtaka au kumpa uwezo mtumishi yoyote wa Serikali kufanya kitendo au kitu chochote, au vyenginevyo yanamhusu kwa mujibu wa wadhifa wake, yanajumuisha watakaomfuata katika dhamana hiyo na msaidizi wake au wasaidizi wake.

(4) Pale uwezo unapotolewa au kazi inapotakiwa kufanywa na kiongozi wa ofisi, uwezo huo unaweza kutekelezwa na kazi hiyo itatendwa na mtu ambaye kwa wakati huo ni mdhamana wa kutekeleza uwezo na kazi hizo za ofisi.

Uwezo wa Rais kufuta amri.

64. Rais anaweza kufuta amri yoyote chini ya kifungu cha 63(1)(a) na akaamrisha mtu wa aina hiyo steuliwe au arudishwe tena mara moja.

Ila ifahamike tu kwamba katika uteuzi huo au kurejeshwa tena huko Rais anaweza:-

- (a) akaamuru kwamba mshahara wake katika kipindi alichochishwa au kuondoshwa au kusimamishwa vyevyote iwavyo, utafishwe; au
- (b) akaamuru kwamba zile siku ambazo alischishwa, aliondoshwa au alisimamishwa zihesabike kama ni likizo bila ya malipo; au
- (c) akatoa shuruti nyengine kama atavyoona inafaa katika amri yake hiyo.

SEHEMU YA X

MCHANGANYIKO

Usawazishaji
wa makosa.

65. Ikiwa kuna makosa yoyote ya usajili au uchapishaji wa Muswada au sheria yoyote katika Gazeti, Mwanasheria Mkuu au ofisa mwingine wa sheria, anaweza, kwa amri katika Gazeti, kutos maelekezo yatakayosawazisha kosa kama hilo na maelekezo yote yatasomeka pamoja na Muswada au Sheria inayohusikana nayo, na Muswada au Sheria ya namna hiyo, kuanzia tarehe ya mwanzo kuchapishwa, itsanza kufanya kazi kama vile ilivyosawazishwa.

Kubadilika
kwa hati.

66. Isipokuwa kama itaelezwa vyengine, wakati wowote ambapo hati yoyote imeelekezwa na sheria yoyote, chombo au waraka ambao unatakiwa uwe katika umbile fulani, waraka huo au hati haitakuwa batili kwa sababu ya mabadiliko madogo madogo ambayo hayatabadilisha maana hasa ya hati hiyo.

Uwingi.

67. Pale kitu kinapotakiwa au kuhitajika kufanywa na zaidi ya watu wawili, wingi wao wanaweza kukifanya.

Uwezo wa
Bodi
kuathirika
na nafasi
wazi.

68. Ikiwa kwa su chini ya sheria yoyote, Bodi, Kamisheni, Kamitii, au chombo kinachofanana na hivyo, uwezo wa Bodi kama hiyo, Kamisheni, Kamitii, au chombo kinachofanana na hivyo, hakitaathiriwa kwa:-

- (a) nafasi iliyowazi katika wanasachama wake;
- (b) kugunduliwa baadaye kwamba kulikuwa na hitilafu au makosa katika uteuzi au sifa za mtu ambaye alikuwa ni mwanasachama wake,

ila tu pale ambapo maelezo yatahitajia vyenginevyo.

Kuhifadhika
haki za
Serikali.

69. Hakuna sheria ambayo, katika njia yoyote ile, itakayoweza kuathiri haki za Serikali isipokuwa kama itaelezwa wazi ndani yake au isipokuwa ionekane, katika umuhimu wa matumizi, kwamba Serikali inalazimika kuifusta.

Sheria kuihusu
Serikali.


70. Sheria hii itaihusu Serikali.

Kufutwa
kwa Sheria
ya Tafsiri
ya 1953,
pamoja na
Nam. 1/1964.

71. (1) Sheria ya Tafsiri ya 1953, Sura ya I ya Sheria za Zanzibar pamoja na Sheria Nambari 1 ya 1964 zinafutwa.

(2) Sheria ndogo yoyote iliyoungwa chini ya sheria hizo zilizofutwa zitsendelea kutumika kama ni sheria ndogo iliyoungwa kwa mujibu wa vifungu vya sheria hii.

Inepitishwa katika Baraza la Wawakilishi tarehe 10 Oktoba, 1984.


IDI P. HASSAN
KATIBU
BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR.